


ASb
approved



Basi Kubwa La Bluu

Brigid Simiyu

Mango Tree

Kiswahili






Kulikuwa na basi moja tu katika kijiji cha Ebei. Lilikuwa basi kubwa lenye rangi ya bluu. Lilinguruma sana.



Siku moja mamake Ebei alisema, "Kesho tutaenda mjini
kununua sare yako ya shule."



Ebei alifurahi sana. Kumbe atasafiri katika lile basi kubwa la bluuu! Usiku huo hakuweza kulala vizuri.



Mamake alipoenda kumuamsha, Ebei alikuwa tayari amevaa.



Ebei na mamake walienda kwenye kituo cha basi. Walisubiri
lile basi kubwa la bluu. Basi halikufika.



Watu wengine walifika kwenye kituo cha basi. Wote walilalamika kuwa basi lilichelewa. Mmoja aliuliza, "Basi limetuacha?"



Ebei alikuwa na wasiswasi. "Tusipokwenda mjini, sitapata sare yangu ya shule," aliwaza.




Baadhi yao walikata tamaa wakarudi nyumbani. Lakini Ebei alilia akakataa kurudi. "Tutasubiri zaidi," mamake alimtuliza.



Ghafla, waliskia mngurumo. Wakaona vumbi hewani. Basi
lilikuwa linakuja kwa kasi.



Basi halikuwa la bluu wala halikuwa kubwa. Basi lile lilikuwa dogo na jekundu. Waliosubiri waliliangalia tu na hawakuingia ndani.



Dereva aliwaita, "Ingieni! Ingieni!
Tumechelewa sana leo."



Ebei na mamake walikuwa wa kwanza kuingia. Mara wote
waliingia ndani ya basi lile dogo jekundu.



Ebei alichungulia dirishani. Aliwaona watu wengi zaidi
wakiingia ndani ya basi.



Mara basi likaondoka. Ebei aliwaona watu wengine wakikimbia kulifikia basi. Walikuwa tayari wamechelewa.



Mamake Ebei alimwuliza dereva, "Liko wapi basi kubwa la bluu?" Dereva alimjibu, "Samahani mama, basi la bluu liliharibika. Linatengenezwa. Kesho litakuja."



Ebei hakujali rangi wala ukubwa wabasi. Alifurahi kuwa basi lile likuwa linawapeleka mjini. Hatimaye, atanunuliwa sare ya shule.

You are free to download, copy, translate or adapt this story
and use the illustrations as long as you attribute in the
following way: Mecelin Kakoro Author - Mecelin Kakoro

Translation - Brigid Simiyu

Illustration - Mango Tree

Language - Kiswahili

Level - First sentences © African Storybook Initiative 2015

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org

